

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA THELATHINI NA TATU**

**25 MEI, 2023**



## **ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

---

### **MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA THELATHINI NA TATU – TAREHE 25 MEI, 2023**

#### **I. DUA:**

#### **II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

#### **WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

#### **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **429. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaongeza majengo katika Kituo cha Afya cha Matamba Wilayani Makete.

##### **430. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Vituo vya Afya kwenye Kata zilizopo pembezoni mwa Tabora Mjini.

##### **431. MHESHIMIWA ROBERT CHACHA MABOTO (BUNDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itabainisha mipaka ya Kata ya Wariku – Bunda Mjini.

## **432. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE (TABORA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga vyumba maalum vyakuseweka mitambo ya X – Ray na *Ultra Sound* katika Kituo cha Afya Upuge.

## **OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

## **433. MHESHIMIWA ISSA JUMANNE MTEMVU (KIBAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, nini mkakati wa kushughulikia malalamiko ya ajira za Kada ya Afya na Elimu kutolewa kwa Waombaji wanaotoka baadhi ya maeneo.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

## **434. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Tarafa za Kitumbeine na Engarenaibor hususan kwenye Migodi ya Rubi.

## **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

### **435. MHESHIMIWA TUMAINI BRYCESON MAGESSA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha Wavuvi ambao wameunda vikundi na kuanza ufugaji wa vizimba katika Jimbo la Busanda.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **436. MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL SICHALWE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua migogoro kati ya Wananchi na maeneo ya Hifadhi za Taifa ikiwemo Jimbo la Mombasa.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **437. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Nangurukuru - Liwale.

#### **438. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Bandari ya Karema itafunguliwa na kuanza kufanya kazi kwa kuwa ujenzi umekamilika kwa asilimia 87.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupidisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**DODOMA  
25 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**